**TAMKO LA BARAZA KUU LA WAISLAMU WA TANZANIA NA TAASISI ZOTE ZA KIISLAMU NCHINI JUU YA YALE YALIYOTOKEA WAKATI NA BAADA YA UCHAGUZI WA OKTOBA 29, 2025**

Assalaam alaykum warahmatullahi wabarakaatuh.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mola wetu Muumba na kumtakia rehma na amani kiongozi wetu Bwana Mtume, Muhammad, Swala na salamu zimuendee yeye, maswahaba wake pamoja na watu wa nyumbani kwake.

Hivi karibuni taifa letu lilifanya uchaguzi mkuu wa kumchagua Raisi wa Jamhuri ya muungano, Raisi wa Zanzibar, Wabunge,vwawakilishi pamoja na Madiwani. Katika kipindi chote cha mchakato wa kuendea uchaguzi huu tumeshuhudia kwa upande wa wanasiasa kuibuka kwa makundi mawili kwa ukubwa tofauti.

Kundi moja likitaka uchaguzi ufanyike kwa mujibu wa katiba ya nchi yetu inavyotutaka.

kundi la pili likigomea kushiriki na kutaka wengine wote wasishiriki kutokana na kile walichokuwa wanakieleza madai ya mabadiliko waliyokuwa wanayataka yafanywe kwa namna wanavyotaka wao.

Na kutokana na hali hii kundi hili mpaka tulipoingia kwenye uchaguzi wao hawakushiriki katika uchaguzi wetu wa mwaka huu 2025.

Tarehe 29 Octoba ndio siku iliyokuwa ya kupiga kura na kura zilipigwa na uongozi kupatikana.

Kuanzia siku ile ya kupiga kura kulizuka genge lililokuwa likiwatisha watu kwa kupora na kuharibu mali pamoja na miundo mbinu mbalimbali, kuchoma moto vituo vya mafuta pamoja na ofisi za umma.

Katika siku hizi za uhalifu huu Watanzania wakagawika katika makundi yafuatayo;

- Kundi la waliofanya uhalifu.
- Waliochukizwa na uhalifu uliokuwa ukifanywa.
- Kundi la waliofurahia uhalifu na uvunjifu wa amani uliotokea.
- Kundi la wachochezi wa ndani na nje ya nchi yetu, wakiwemo mpaka wale ambao si watanzania.
- Serikali na vyombo vya dola.
- Wanasiasa kwa mitazamo tofauti.

Wakati haya yakiendelea vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vilitoa tamko kuhusu kile kilichokuwa kinaendelea.

Mkuu wa Majeshi nchini alitufahamisha kuwa kile kilichokuwa kinaendelea ni uhalifu na watekelezaji wa uhalifu huo ni wahalifu na hapa nanukuu;

"Ndugu wananchi itakumbukwa kuwa jana tarehe tarehe 29 oktoba 2025 nchi yetu ilikuwa na zoezi la Uchaguzi Mkuu. Wakati zoezi hilo likiendelea kulitokea vitendo vya kihalifu, vilivyotekelezwa na baadhi ya watu wahalifu,wasiolitakia mema taifa letu katika maeneo mbalimbali ya nchi, vitendo hivyo vilihusisha uharibifu wa miundo mbinu ya umma, mali za umma na za watu binafsi. Vitendo hivyo ni uhalifu usiokubalika ambao lazima ukomeshwe mara moja". Mwisho wa kunukuu.

Kutokana na vitendo hivi vya kihalifu ambavyo vililazimu vyombo vyetu vya usalama kudhibiti hali hiyo, ndani yake kukatokea vifo vya watu wasio na hatia na wengine kupata ulemavu wa kudumu pamoja na uharibifu, wizi na upotevu wa mali.

Yote haya yakisababishwa na hilo genge lilokuwa likifanya fujo, wizi na uharibifu mkubwa wa mali na miundo mbinu.

Sisi kwa umoja wetu tunalaani vitendo hivi vya kihalifu ambavyo udhibiti wake umepelekea vifo vya watu wasio na hatia.

Sisi kwa umoja wetu tumeumia sana kwa haya yaliyotokea hasa maisha ya watu yaliyopotea kutokana na vitendo hivi vya kihalifu.

Kwani mafundisho yetu yanasema maisha ya mtu mmoja kupotea ni sawa na kupotea maisha ya watu wote.

Qur'ani Surat Al-Maida aya 32.

Kama ambavyo katika aya hii pia inaeleza yeyote mwenye kuokoa maisha ya mtu mmoja ni sawa ameokoa maisha ya watu wote.

Kwa msingi huu sisi kwa umoja wetu tumesikitishwa sana na upoteaji wa maisha ya watu kwa hali yoyote ile iwayo.

Na ndio maana kwa sababu ya kuchelea mambo kama haya sisi kwa umoja wetu kipindi cha kabla ya uchaguzi tumefanya kazi kubwa ya kuhimiza juu ya umuhimu wa kutunza amani ya nchi yetu na pale inapobidi kuna haki zinadaiwa basi haki hizo zidaiwe katika taratibu

ambazo hazitoleta uvunjifu wa amani na kupelekea maafa makubwa kama haya yaliyotokea katika nchi yetu.

Kabla ya zoezi la uchaguzi mkuu tulitumia muda mwingi kuwaasa waumini wetu na watanzania kwa ujumla kuitunza na kuilinda amani ya nchi yetu pamoja na kujiepusha na vitendo na maneno ambayo yanaweza kuwa cheche ya kupelekea uvunjifu wa amani.

Sisi kwa umoja wetu tunaendelea kushikilia msimamo wetu wa kujali na kusimamia na kuilinda amani ya nchi yetu. Kwani tunaamini pahala pasipo na amani haki haiwezi kudaiwa wala kupatikana.

Haki ni mchakato (Process) na kwa msingi huu haki ili ipatikane inahitaji wakati na pahala (time and space) na ili pahala pa kudaia haki paweze kufanya hivyo amani inahitajika kwanza ndipo haki iweze kupatikana.

Pahala penye fujo, vurugu na watu kutishiwa mpaka kukatwa sehemu za miili yao,pahala hapo kamwe hapawezi kuwa na mazingira sahihi ya kutoa hiyo haki inayodaiwa.

Sisi kwa umoja wetu tunaamini vitendo hivi ambavyo vimeleta maafa katika nchi yetu ni vitendo vya kulaaniwa na ni lazima vidhibitiwe na kuhakikisha havitokei tena katika nchi yetu.

Lakini pia sisi kwa umoja wetu tunaitaka serikali yetu ifanye uchunguzi wa kina juu ya kina nani ndio walikuwa vinara wa kuwachochea vijana wetu katika kufanya uharibifu huu mkubwa kuwahi kutokea katika nchi yetu mpaka kufikia maisha ya watu kupotea.

Sisi kwa umoja wetu tunaiomba serikali yetu kuwaangalia wale wote ambao kwa namna moja ama nyengine wamekumbwa na maafa haya na wala hawakuhusika kwa namna yoyote ile, kuwaangalia kwa jicho la huruma pamoja na kuwafariji.

Sisi kwa umoja wetu tunaisihi Serikali katika kipindi hiki iangalie pale panapohitaji suluhu pafanyike suluhu kama mafundisho yetu yanavyosema " Na suluhu ni kheri". Surat Annisaa aya ya 128.

Na pale panapohitaji maridhiano basi pia Serikali yetu iwe tayari kufanya hivyo kwa maslahi mapana ya nchi yetu na raia wake.

Japokuwa pia tunaisihi Serikali yetu suluhu na maridhiano isiwe ni zawadi wanayopewa wale waliohusika na kushiriki katika uhalifu huu uliopelekea maafa haya.

Sisi kwa umoja wetu tumekusanyika hapa kwa lengo la kumuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuilinda nchi yetu na watu waovu na awasamehe wale ambao hawajui walifanyalo lakini wale waliofariki na wasio na hatia awalipe kwa namna apendavyo kwa hakika yeye ni mwingi wa rehema na kurehemu.

Na mwisho sisi kwa umoja wetu hatuoni kuwa ni busara na hatuoni kuwa ni afya kwa umoja wetu na mshikamano wetu katika nchi yetu sisi kuitwa wajinga kwa sababu tu tulikuwa tukihimiza amani.

Sisi kama sehemu ya jamii katika nchi yetu siku zote tumekuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kuhimiza amani katika nchi yetu hata pale ambapo kufanya hivyo kunapokuwa kunatulazimu kukubali maumivu makubwa lakini tulikuwa tayari kufanya hivyo.

Tunataka tueleweke na viongozi wa dini wenzetu kuwa sisi sio wajinga na hatuwezi kuwa wajinga kwa sababu ya kuzungumzia na kuhimiza amani.

Kama ambavyo kiongozi wetu mheshimiwa Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania pamoja na viongozi wengine kamwe hawezi kuwa wajinga kwa sababu ya kusimamia suala la amani katika nchi yetu, amani ambayo ikiwepo tunanufaika na kufaidika nayo sisi sote.

**Ifahamike pia kuwa sisi kwa umoja wetu tukiongozwa na kiongozi wetu mkuu wa kiimani hatujawahi hata mara moja kuzuia watu wasidai haki zao wala kufuatilia haki zao kwa kufuata taratibu tulizojiwekea katika nchi yetu.**

**Sisi kwa umoja wetu tunaamini kuwa ndani ya nchi yetu kuna haki mbalimbali ambazo zinadaiwa kutoka kwa makundi mbalimbali na wakati mwengine kutoka kwa mtu mmoja mmoja.**

**Na kwa hivyo tunawaasa wale wote wanaojiona kuwa wanazo haki wanazodai kutoka serikalini au kokote kule ndani ya nchi yetu,hata mara moja kudai haki hizo isiwe sababu ya kufanya vitendo vya kihalifu na kudhuru wengine.**

**Mafundisho ya dini yetu yanatutaka mara zote tuhakikishe kuwa hatumdhuru yeyote na wala sisi wenyewe tusijidhuru.**

**Amesema Bwana Mtume,swala na salamu zimuendee;**

**"Usidhuru wala Usidhurike".**

Tunasisitiza kuheshimiana, kuthaminiana na kusimama pamoja katika kudumisha amani,umoja na mshikamano wetu bila ya upande fulani kujiona kuwa wao ndio wana haki zaidi na nchi hii kuliko wengine.

Kama ambavyo sisi kwa umoja wetu tunaamini kwa dhati kuwa katika nchi yetu hakuna raia daraja la pili kwa sababu ya dini,kabila,wanakotoka au rangi yao.

**MWISHO**

Sisi kwa umoja wetu tunaazimia kuendelea kuiombea dua nchi yetu dhidi ya wale wote wanaotaka amani ya nchi hii ipotee kwa maslahi yao na Mwenyezi Mungu atubainishie wale waovu tuwajue na kuwatambua na atuoneshe haki katika sura yake ya kweli na aturuzuku kuifuata na atuoneshe batili katika vazi lake la uovu ili tuweze kuisitisha.

Aidha mwisho tunatoa pongezi kwa Mhe. RAis, Makamu wa Rais, Spika wa Bunge, Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wabunge, wawakilishi na Madiwani kwa kuchaguliwa kuwa viongozi wetu kwa miaka mitano ijayo.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu aijaalie nchi yetu idumu amani amani yake, awajaalie wale wote waliathirika na maafa haya awape faraja na kuwaondoshea huzuni katika nyoyo zao,ajaalie wale walipoteza Maisha awape malipo yanayowastahiki huku walipo na wale waliopata majeraha awaponye majeraha yao kwa haraka na walipoteza mali zao Mwenyezi Mungu awape badali.

Allahumma Ameen.

Tunatoa wito kwa Waislamu na Watanzania wote katika kudumisha amani,mshikamano na umoja wetu wa kitaifa kwani kufanya hivi kuna maslahi kwetu sote.

1. Sheikh Hassan Said Chizenga – Katibu wa Baraza la Ulamaa BAKWATA
2. Sheikh Abdallah Ndauga – Mwenyekiti Hay'atul – Ulama
3. Sheikh Alhad Mussa Salum – Mwenyeiti JUWAQUTA Taifa
4. Sheikh Rajab Katiba – Katibu Mkuu – Al-Mallid
5. Amir Khamis Mbwana – Katibu Mkuu wa Umoja wa Maimamu (UMATA)
6. Amir Khalfan Mohamedi – Naibu Katibu – Darul Irishad Markaz Tabligh
7. Ustaadh Juma Nchia – TAMRO – Mwakilishi

IMETOLEWA LEO ALHAMIS TAREHE 13/11/2025.